JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA**

PPRA
Public Procurement Regulatory Authority

**Kumb. Na. FB.192/247/01/B/27** **21 Julai, 2026**

**Kwa Taasisi Nunuzi zote na Wadau wa Ununuzi wa Umma**

**YAH: KALENDA YA MAFUNZO YA MATUMIZI YA SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA YA MWAKA 2023 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2024 NA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA UNUNUZI WA UMMA (NeST) KWA MWAKA 2026/2027**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, pamoja na majukumu mengine, inalo jukumu la kuanzisha, kuendeleza, kutunza na kuhuisha mfumo wa kuwezesha ununuzi wa umma kwa njia ya teknolojia za habari na mawasiliano ikijumuisha matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika usimamizi wa ununuzi na ugavi. Aidha, Mamlaka inalojukumu pia la kujenga uwezo kwa wadau wanaohusika na masuala ya ununuzi na ugavi wa umma.

3. Hivyo, kufuatia maboresho makubwa katika Sheria ya Ununuzi wa umma ya mwaka 2023 pamoja na kutengenezwa na kuboreshwa kwa moduli za Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST), Mamlaka imeandaa Kalenda ya Mafunzo ya mwaka 2026/2027 ambayo itaanza kutumika Mwezi Agosti, 2026. Kwa barua hii Mamlaka inatangaza ratiba ya Mafunzo kutokana na mahitaji ya watumiaji kama inavyoonekana kwenye ratiba iliyoambatanishwa.

4. Mafunzo ya pamoja ya kutumia mfumo yatatolewa kwa washiriki kulingana na muda uliopangwa kama ifuatavyo:

(a) Mafunzo kwa taasisi nunuzi yatatolewa kwa siku tano (5) kwa ada ya TZS 600,000.00

(b) Mafunzo kwa wazabuni yatatolewa kwa siku moja (1) kwa ada ya TZS 100,000.00

(c) Mafunzo kwa Wakuu wa Taasisi na Bodi za Wakurugenzi yatatolewa kwa siku mbili (2) kwa ada ya TZS 1,500,000.00

(d) Mafunzo maalumu kwa watumishi (Boot camps) yatatolewa kwa siku kumi (10) kwa ada ya TZS 1,200,000.00

5. Maafisa Masuuli wanahimizwa kushiriki mafunzo haya na kuwaruhusu watumishi wao kuhudhuria mafunzo watakayochagua kushiriki kwa mujibu wa Kalenda ya Mafunzo iliyoambatanishwa pamoja na mwaliko huu, ambayo pia inapatikana katika tovuti ya PPRA kupitia www.ppra.go.tz na mfumo wa mafunzo unaopatikana kupitia https://tsms.ppra.go.tz

6. Ili kushiriki mafunzo, kila mshiriki anapaswa kujisajili katika mfumo wa mafunzo (https://tsms.ppra.go.tz), kwa kuchagua mafunzo anayotaka kushiriki na kuthibitisha ushiriki kwa kulipia ada ya mafunzo kupitia Namba ya Malipo (Control Number) inayotolewa na mfumo wa mafunzo (tsms) kulingana na aina ya mafunzo husika. Iwapo taasisi itahitaji Namba ya malipo ya pamoja kwa washiriki zaidi ya mmoja, huduma hii inapatikana katika mfumo wa mafunzo wa (TSMS) eneo la "Group Bill".

7. Tunashukuru kwa ushirikiano wenu.

Dennis K. Simba
**MKURUGENZI MKUU**